

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA GEITA

MKOA WA GEITA

Simu No. 0282520437

Nukushi No. 0282520437

Barua pepe : td.geitac.go.tz



Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji wa Geita,
P.O Box 384,
Geita.
20/04/2018.

**CHINI YA KIFUNGU 11(1) CHA SHERIA NA. 2 YA KODI YA MAJENGO YA MWAKA
1983 PAMOJA NA MAREKEBISHO YA MWAKA 2000, 2016 NA 2017**

1. Tangazo ili litanukuliwa kama Tangazo la Mamlaka ya Mapato Tanzania ikishirikiana na Halmashauri ya Mji wa Geita la kuweka jedwali la Uthamini wa majengo kwa ajili ya Ukaguzi, Tangazo la mwaka 2018.
2. Wananchi wanaarifiwa kwamba, jedwali la uthamini wa majengo liloandaliwa na Halmashauri ya Mji wa Geita kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania limewekwa katika Ofisi za Mji, Ukumbi wa Gedeko Geita kwa ajili ya wananchi kukagua taarifa za majengo yao yaliyoainishwa katika jedwali la Uthamini la mwaka 2017 kwa kata zifuatazo; Kalangalala, Buhalahala, Mtakuja, Bombambili na Nyankumbu kwa majengo yalifanyiwa uthamini.
3. Wanachi wanajulishwa kwamba mtu yeyote anaweza ndani ya siku ishirini na nane (28) tangu tarehe ya tangazo hili, kukagua jedwali la uthamini wa mwaka 2017 muda wa saa za kazi na kuchukua viziduo.
4. (i) Mtu yeyote anaweza kutoa pingamizi kuhusiana na jedwali la uthamini wa majengo mwaka 2017 na kuandika kwenye fomu maalumu ambazo zinapatikana kwenye ofisi ya Mthamini wa Mji kuanzia tarehe 2 May 2018
(ii) Mtu yeyote hataruhusiwa kuweka pingamizi lolote baada ya Baraza huru la Uthamini kukamilisha kazi yake. Utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa tangazo hili uzingatiwe.
5. Pingamizi lolote lililowekwa kwa maandishi maalumu sharti lirudishwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita wakati wa saa za kazi 1:30 asubuhi mpaka 9:30 alasiri) kuanzia tarehe 2 May 2018.
6. Mtu yeyote aliyeweka pingamizi kwa mujibu wa aya ya 4 ya tangazo hili anaweza, muda wowote kabla ya tarehe 29 May 2018 katika saa za kazi (1:30 asubuhi mpaka 9:30 alasiri) kuondoa pingamizilake kwa kujaza fomu maalumu inayopatikana kwenye ofisi za mthamini wa Mji.
7. Baraza huru la Uthamini wa kodi ya majengo litakutana kwa madhumuni ya kupitia pingamizi kuhusiana na jedwali la Uthamini wa Majengo mwaka 2017 ndani ya siku tatu (3) kuanzia tarehe 30 May 2018.
8. Tarehe 06 June 2018 imeteuliwa kuwa tarehe rasmi ya kuanza kutumika kwa jedwali la uthamini wa majengo 2017 na tarehe hiyo imeteuliwa kama tarehe rasmi ya uthamini kwa madhumuni ya sehemu 11(i) (d) na 11(e) ya sheria ya Kodi ya Majengo.

Modest J. Appollinary
MKURUGENZI WA MJI
GEITA